

Taarifa kuhusu Haki na Majukumu yako kama Mshiriki wa WIC

1. Viwango vya kustahiki na kushiriki ni sawa kwa kila mtu haijalishi umbari, rangi, asili ya kitaifa, umri, jinsia au ulemavu.
2. Ninaweza kukata rufaa ya uamuzi wowote uliofanywa na WIC kuhusu mtoto wangu au kustahiki kwangu.
3. Nitapokea maelezo ya lishe na rufaa za huduma za afya. Ninahimizwa kushiriki katika huduma hizi.
4. Nitapokea maagizo kuhusu jinsi ya kutumia hundi za cheki za WIC.
5. Nitazingatia miadi yangu ya WIC. Nikishindwa kuchukua hundi zangu za cheki za WIC kwa miezi mitatu (3) ikifuatana, ninaweza kuondolewa kwenye Mpango huu.
6. Nitashiriki tu katika kliniki moja ya WIC kwa wakati mmoja. Ninaelewa kwamba ni kinyume cha sheria kuandikishwa katika zaidi ya kliniki moja kwa wakati mmoja, aidha katika Pennsylvania au katika jimbo lingine. Kupokea hundi za cheki za WIC kutoka kwa kliniki mbili za WIC au majimbo mawili katika mwezi mmoja kutasababisha kuondolewa kwenye Mpango.
7. Washiriki wa WIC wanaouza au kubadilisha vyakula au fomyula zilizounuliwa kwa siri (ambazo hazijanunuliwa kwa kutumia hundi ya cheki ya WIC) ambazo zinafanana na chakula na fomyula walizoagizwa wanunue na Mpango wa WIC lazima wabakie na risiti ya vitu hivyo ili wakiombwa na Mpango wa WIC waweze kuthibitisha kwamba hawauzi au kubadilisha vyakula na fomyula zilizotolewa na Mpango wa WIC.
8. Una haki ya kuwasilisha malalamiko dhidi ya duka la rejareja kwa kuwasiliana na Mratibu wa Duka la Rejareja la Shirika la Ndani. Unaweza kuchagua kutojulikana.
9. Waombaji/waidhinishaji na watu wanaostahiki wamelindwa chini ya ADA au Sehemu ya 504. Ikiwa unahisi haki hizi zimekiukwa una haki ya kuwasilisha malalamiko. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu sheria hizi au jinsi ya kuwasilisha malalamiko, wasiliana na mratibu katika Shirika la Serikali, nambari ya simu (717)783-1289.

Nimesoma haki na majukumu yangu. Ninakiri kwamba maelezo niliyoyatoa kwa WIC ni sahihi kwa ufahamu wangu wote. Fomu hii inawasilishwa kuhusiana na risiti ya usaidizi wa Serikali. Huenda WIC ikathibitisha maelezo yoyote kwenye fomu hii. Ninaelewa kwamba kutoa maelezo ya uongo au ya kupotosha kunaweza kusababisha kulipa WIC, *pesa taslimu*, thamani ya faida za chakula nilizopewa kimakosa. Pia, ninaweza kushtakiwa kwa makosa kiraia na ya jinai chini ya sheria za Jimbo na Serikali. Ninaelewa kwamba Katibu wa Afya anaweza kuruhusu kutolewa kwa maelezo ambayo nimeyatoa kwa WIC kwa mipango mingine kama vile CHIP, Usaidizi wa Matibabu, SPAN, Kiamsha Kinywa cha Shule na Chakula cha Mchana cha Shuleni. Maelezo haya yatatumika tu ii kubainisha kustahiki kwangu katika mipango hii na kwa ufikiaji. Ninaelewa kwamba faili yangu au faili ya mtoto wangu inaaweza kupitiwa na mkaguzi mwingine (asiye wa WIC) kama sehemu ya ukaguzi wa kila mwaka wa WIC. Maelezo yote ni ya siri.

Ninathibitisha kwamba nimepokea, nimesoma na kukubali kufuata Kanuni za Mpango wa WIC.

Swahili - WIC Rights and Responsibilities